

**Swahili transcript:**

Tanzania tuna mavazi ya aina nyingi, tuna vazi la batiki, tuna vazi la kanga. Na tunavaa kanga katika maeneo mbalimbali, kwa mfano hii niliyovaa hii ni kanga, lakini imechanganywa na hiki kitambaa cheupe ambacho ni bazee, tunaita bazee. Kwa hiyo tunashona pia kanga, kanga tunaweza tukavaa kama zilivyo na wakati mwingine pia tunashona kanga. Kwa mfano hapa nguo hii niliyovaa, mara nyingi nguo kama hii tunavaa katika sherehe za kitchen party. Sherehe ya kitchen party ni sherehe ambayo inamwandaa binti ambaye anategemea kuolewa, ni sherehe ambayo wakina mama ndio ambao wanaiandaa sherehe hii. Kwa hiyo vazi hili la kanga, hii ni kanga ambayo imechanganywa na kitambaa hiki cha bazee, kwa hiyo hii ni kanga, kama mnavyoiana hii pia ni kanga lakini imeshonwa. Ona imetengenezwa, imechanganywa sehemu mbalimbali, na kama nilivyosema vazi kama hili mara nyingi tunavaa katika sherehe mbalimbali, kama sherehe ya kitchen party ninaweza nikavaa vazi la aina hii. Kwa hiyo watanzania wana mavazi mengi na kama nilivyosema mwanzoni kuna mavazi mengi ya kila aina, na inategemea na jinsi wewe mwenyewe unavyotaka nguo yako ishonwe. Kwa sababu unakwenda kwa fundi cherehani na unamweleza mimi nguo yangu nataka ishonwe hivi na hivi. Kwa hiyo yule fundi anachukua vipimo, anakupima vizuri, anakuja anachukua ile kanga pamoja na kitambaa ambacho unataka kichanganywe na ile kanga. Kwa hiyo anatengeneza nguo ambayo wewe unaitaka. Vazi la kanga na mashono ni tofauti na sehemu nyingine ambazo ukitaka nguo labda lazima ukanunue nguo ambayo tayari imetengenezwa kiwandani. Lakini kwa Tanzania tunayo bahati hiyo kwamba nguo ambayo wewe unataka, ndio ambayo fundi anakushonea. Kwa hiyo unanunua kitambaa au unanunua kanga yako pamoja na kitambaa chako cha bazee, na fundi anavishona sawasawa na jinsi wewe unapenda. Kwa hiyo kama mnavyoona ni vazi ambalo ni zuri na linapendeza kwa kweli na linavutia.

### **English translation:**

In Tanzania, we have different kinds of dresses. We have *batiki*, and we have *kanga*. We wear *kanga* on different occasions. For example, this is a *kanga* but it has been combined with this white cloth, called *bazee*. We call it *bazee*. We can wear *kanga* as it is, and sometimes we bring it to the tailors to make trousers, skirts, or gowns. For example, this kind of dress which I am wearing; we would normally wear to kitchen parties. A kitchen party is a kind of celebration to prepare a young woman who is about to get married. Women are the ones who have this party. As you can see, this is *kanga* that has been combined with *bazee* cloth. It has been combined in different places, and as I said earlier, this is the kind of dress we wear to ceremonies such as a kitchen party. So we Tanzanians have different kinds of dresses. It also depends on what you want your dress to look like. You go to the tailor and tell her or him what you want your dress to look like. Then the tailor takes some measurements and makes your dress. So we Tanzanians are lucky because we can make our own dresses. That is different from other countries where, when you want a dress, you have to buy it ready made. You buy *kanga* and *bazee* cloth which you want to use along with your *kanga*, then a tailor makes your clothes the way you like them. So *kanga* is a good style, and you look good when you wear it.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated